**KIS 213- PRE 20TH CENTURY KISWAHILI POETRY**

**2ND YEAR SECOND SEMESTER- 2013/2014 ACADEMIC YEAR**

**MAIN EXAM: REGULAR**

MAAGIZO: JIBU MASWALI MANNE: SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA

1. (a) Fafanua sifa za tanzu zifuatazo za ushairi kabla karne ya ishirini (alama 15)
   (i) Takhmisa
   (ii) Tumbuizo
   (iii) Nyimbo
   (iv) Tenzi
   (v) Mashairi

   (b) Kwa kutumia mifano yoyote ya ushairi wa kabla karne ya 20, jadili dhima ya ushairi katika jamii (alama 10)

2. Inkishafi ni utenzi uliopitwa na wakati. Jadili (alama 15)

3. Kwa kuzingatia matapo matatu ya wanafasihi, jadili maudhui yaliyoshughulikiwa katika Utenzi wa Mwanakupona (alama 15)

4. Fafanua kwa kina maudhui yoyote matano yanayojitokeza katika utenzi wa Fumo Liyongo (alama 15)

5. Ushairi wa Muyaka ni dhihirisho tosha la jinsi ushairi wa jadi ulitoka msikitini na kuingia sokoni. Tathmini kauli hii kwa kuzingatia maudhui yoyote matano kutoka katika ushairi huo. (alama 15)

6. Tathmini shairi lifuatalo kwa kuzingatia fani na maudhui (alama 15)

TWANGALIANA KWA MATO

Yaulizeni ya leo, mkumbuke na ya jana
Mambo jinsi yendao ,hugeuka wat'u nia!
Wavyele huwa vijana, mambo yakiwatatia!
Ambapo yawele haya; twangaliana kwa mato

Twachana kuambiana, nenole limepotea
Zamani zikidangana, hugeuka wat'u nia
Wavyele huwa vijana, mambo yakiwatatia
Ambapo yawele haya; twangaliana kwa mato.

Ambapo yawele haya, msinene ni maovu
Ipese kuzingatia, msiitwe wapumbavu
Huwaje kuata ndia, mkashika ushupavu
Huo ndio potevu; twangaliana kwa mato

Huo ndio upotevu, wa kujitia mwituni
Na ndia ya ulekevu, si kwamba hamuioni!
Vitendo vya nguvunguvu, mambo yakwe hayafani
Leo pana jambo gani? Twangaliana kwa mato!

**KIS 213- PRE 20TH CENTURY KISWAHILI POETRY**

**2ND YEAR SECOND SEMESTER- 2013/2014 ACADEMIC YEAR**

**SUPPLIMENTARY/ SPECIAL**

MAAGIZO: JIBU MASWALI MANNE: SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA

1. (a) Dhima ya kazi za fasihi hutegemea wakati na muktadha. Jadili kauli hii kwa kurejelea utenzi wa Mwanakupona(alama 15)

   (b) Ushairi kama utanzu wa fasihi una nafasi kubwa katika **jamii ya sasa**. Fafanua kauli hii. (alama 10)

2. Inkishafi ni utungo wa kidini unaovuka mipaka ya dini moja. Jadili (alama 15)
3. Fafanua kwa tafsili, sifa za tanzu zozote **tano** za ushairi kabla karne ya ishirini (alama 15)
4. Huku ukirejelea utenzi wa fumo Liyongo, jadili jinsi maudhui ya ushujaa wa Kiafrika unavyojitikeza (alama 15)
5. Jadili maudhui yoyote **tano** aliyoshughulikia Muyaka katika mashairi yake (alama 15)
6. Tathmini shairi lifuatalo kwa kuzingatia fani na maudhui (alama 15)

TWANGALIANA KWA MATO

Yaulizeni ya leo, mkumbuke na ya jana
Mambo jinsi yendao ,hugeuka wat'u nia!
Wavyele huwa vijana, mambo yakiwatatia!
Ambapo yawele haya; twangaliana kwa mato

Twachana kuambiana, nenole limepotea
Zamani zikidangana, hugeuka wat'u nia
Wavyele huwa vijana, mambo yakiwatatia
Ambapo yawele haya; twangaliana kwa mato.

Ambapo yawele haya, msinene ni maovu
Ipese kuzingatia, msiitwe wapumbavu
Huwaje kuata ndia, mkashika ushupavu
Huo ndio potevu; twangaliana kwa mato

Huo ndio upotevu, wa kujitia mwituni
Na ndia ya ulekevu, si kwamba hamuioni!
Vitendo vya nguvunguvu, mambo yakwe hayafani
Leo pana jambo gani? Twangaliana kwa mato!